

01-Utangulizi

Himdi Anastahiki Allaah (سبحانه وتعالى) Rabb wa walimwengu, Rehma na amani zimshukie kipenzi chetu Nabiy Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) na jamaa zake, na Swahaba zake (رضي الله عنهم) na kila mwenye kuwafuata mpaka Siku ya Mwisho.

Elimu ya Tajwiyd ni elimu yenye umuhimu wa upeo wa juu kwani inahusiana na maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى), na hapana shaka kwamba kusoma Qur-aan ni njia bora kabisa ya mja kujikurubisha kwa Rabb wake Mtukufu, na kwamba ni amali yenye fadhila na thawabu nyingi mno zilotajwa katika Qur-aan na Sunnah. Mionganini mwazo ni Hadiyth ya 'Uthmaan bin 'Afaan (رضي الله عنه) ambayo imewaathiri wengi na wakaifanyia kazi maishani mwao:

عَنْ عُثْمَانَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((خَيْرُكُمْ مَنْ تَعْلَمَ الْقُرْآنَ وَعَلَّمَهُ))
Impokelewa kutoka kwa 'Uthmaan bin 'Affaan (رضي الله عنه) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ((Mbora wenu ni yule mwenye kujifunza Qur-aan kisha akaifundisha)) [Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhy, An-Nasaaiy, Abu Daawuwd, Ahmad]

Bila ya shaka ni jambo linalopasa kuazimiwa na kila Muislamu kuwa mionganini mwa wataotunukiwa na kupata hizo fadhila. Nikaona umuhimu wa kuandaa kitabu hiki kitachosaidia katika kueleza na kufahamisha hukmu za Tajwiyd. Nikalenga zaidi kutoa mifano bayana ya kinadharia na kuweka rangi kubainisha herufi na i'raab zinazohusiana na hukmu husika ili msomaji aweze kufikia kuwa na ufahamu mpana wa hukmu za Tajwiyd. Pia nimeweka michoro yenye lengo la kumfanyia wepesi msomaji kuweza kufikia kuzielewa hukmu ambazo si nyepesi kuzielewa kinadharia.

Ni muhimu kwa kila mwenye kutaka kujifunza hukmu za Tajwiyd kuhakikisha kuwa anaanza kusoma na kuielewa milango miwili hii: '**Umuhimu wa Elimu ya Tajwiyd**' na '**Lahnul-Jaliy (Makosa ya dhahiri)**

na Lahnul-khafiy (Makosa ya kufichika); kwani humo nimeelezea na kuweka wazi yale yaliyo muhimu na pia kubainisha yale madhara ya kutokusoma Qur-aan kwa kufuata hukmu za Tajwiyd. Kufanya hivi kutampelekea msomaji kufikia kuipenda fani hii ya Tajwiyd na kuwa na shauku ya kutaka kujifunza kwa lengo la kufikia kuwa mahiri katika kuzitekeleza hukmu zake; jambo litalompelekea kuondokwa na khofu ya kufanya makosa ambayo mengine hugeuka dhambi pindi asipotekeliza katika usomaji wake hukmu za Tajwiyd.

Mtu kusoma kitabu hiki au hukmu za Tajwiyd yeye mwenyewe bila ya mkufunzi hakutompelekea kuweza kuufikia ustadi wa kusoma Qur-aan kwa Tajwiyd; bali mwanafunzi wa Qur-aan inampasa apate Qaariu atayemfunza kwa njia ya ‘talaqqiy’¹.

Namshukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kuniwezesha kukusanya Kitabu hiki cha ‘Al-Hidaayah Katika Ahkaam Za Tajwiyd kwani hakuna Awezeshaye ila Yeye tu:

﴿ وَمَا تَوْفِيقٍ إِلَّا بِاللَّهِ عَلَيْهِ تَوْكِيدُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴾

((Na sipati tawfiq [ya kuyawezesha haya] ila kwa Allaah. Kwake natawakali na Kwake narejea.”)) [Huwud (11 : 88)

Baada ya kumshukuru Allaah (سبحانه وتعالى), shukurani zangu pia kwa Abuu Faatwimah ambaye ameipitia kazi hii kadiri alivyowafikishwa. Pia shukurani kwa Al-Akh Muhammad Al-Maawy na Ummu ‘Abdir-Rahmaan. Hali kadhaalika nashukuru familia yangu kwa ujumla kwa kuniunga mkono kwa kila hali katika kufanikisha kazi hii. Allaah (سبحانه وتعالى) Awajaze wote kila la kheri za duniani na Aakhirah. Aamiyn.

Namuomba Allaah (سبحانه وتعالى) kwa khofu na matarajio, Aijaalie kazi hii iwe kwa ajili ya kupata Radhi Zake Pekee na Ajaalie iwe yenyе manufaa kwa ndugu zetu wa Kiislamu na namuomba Atughufurie na Atusamehe kwa makosa yoyote yatakayo kuwemo, kwani juu ya kuwa juhudini kubwa

¹ Kusoma Qaariu mbele ya mwanafunzi uso kwa uso kisha mwanafunzi anamfuutiliza Qiraa-ah chake.

imetendeka katika kukiandaa kitabu hiki, lakini bila shaka yoyote ile, hakitakosa kuwa na kasoro kwa sababu hakuna mkamilifu isipokuwa Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee. Hivyo basi, naomba kwa yejote atakayekitumia akakuta kasoro au akagundua kosa, tafadhali tuandikie kuitia webmaster@alhidaaya.com ili tuweze kurekebisha.

Ummu Iyyaad

15 Muharram 1429 H - 24 Januari 2008 M

Kimehaririwa 1435H - (2014M)

Kimehaririwa tena 1441H (2019M)